

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Simu: +255-26-2323189

Barua pepe: [ps@moha.go.tz](mailto:ps@moha.go.tz)

Tovuti: [www.moha.go.tz](http://www.moha.go.tz)



Mji wa Serikali - Mtumba,

Mtaa wa Habari/Afya,

S.L.P. 2916,

40483 DODOMA.

*Unapojibu tafadhali taja:*

**1 Februari, 2023**

### TAARIFA KWA UMMA

#### ULIPAJI WA ADA KWA JUMUIYA ZA KIRAIA ZILIZOSAJILIWA

#### WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI


Ofisi ya Msajili wa Jumuiya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inazikumbusha Jumuiya za Kidini na zisizokuwa za Kidini zilizosajiliwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kulipa Ada ya Mwaka pamoja na malimbikizo ya ada za miaka ya nyuma kabla ya tarehe 30/6/2023.

Jumuiya za Kidini zinapaswa kulipa Ada ya Shilingi 100,000 na Jumuiya zisizo za Kidini zinapaswa kulipa Ada ya Shilingi 50,000. Aidha, ulipaji wa ada unapaswa kwenda sambamba na uwasilishaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa na Taarifa za Utendaji za Jumuiya hizo kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.

Viongozi wa Jumuiya zote zilizosajiliwa wanakumbushwa na kusesitizwa kutumia Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Jumuiya (RSMIS) unaopatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambayo ni [www.moha.go.tz](http://www.moha.go.tz) kwa ajili ya kulipa Ada za Jumuiya zao au kufika katika Ofisi zetu zilizopo Jengo la Kambarage Ghorofa ya 11 Jijini Dodoma au Jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Ghorofa ya Kwanza Jijini Dar es salaam kwa lengo la kupatiwa huduma stahiki.

Kwa maelekezo zaidi, piga simu namba 0734 712 744 au 0734 712 745.

Imetolewa na:

  
Emmanuel R. M. Kihampa  
**MSAJILI WA JUMUIYA ZA KIRAIA**